Toleo 95 - Jumada al - awwal 1446 H / Disemba 2024

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Uzinduzi wa Kampeni ya Kijamii ya Hizb ut Tahrir / Kenya chini ya Kauli Mbiu: Uislamu Suluhisho Bora la Migogoro ya Kinyumbani

**HABARI NA MAONI**
Kuchaguliwa tena kwa Trump: Mporomoko wa Demokrasia uso Kifani

**MATOLEO**
Udanganyifu wa Chaguo : Kwa nini Upigaji Kura katika Mfumo wa Kisekula Unawabwaga Waislamu

**JIBU LA SWALI**
Hukmu ya Miamala ya Kifedha na Kibiashara kupitia Mtandao wa Intaneti



Afisi ya Habari Kenya

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 04/1446 | Ijumaa, 29 Rabi'al-thani 1446 H | 01/11/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Uzinduzi wa Kampeni ya Kijamii ya Hizb ut Tahrir / Kenya chini ya Kauli Mbiu: Uislamu Suluhisho Bora la Migogoro ya Kinyumbani

Hizb ut Tahrir/Kenya imezindua rasmi kampeni ya kushughulikia masuala ya kijamii ambayo itaendeshwa kwa muda wa mwezi mmoja. Kampeni hii ya mwezi mmoja itaanza tarehe 1 Novemba 2024 na kumalizika tarehe 1 Disemba 2024.

Lengo la kampeni hii ni kuangazia uhalisia wa mfumo wa kijamii wa kibepari na jinsi ulivyosababisha maovu kadhaa ya kijamii katika mujtamaa, ikiwa ni pamoja na kuvunjika kwa ndoa, migogoro ya ardhi, mizozo ya kinyumbani na kiwango kikubwa cha talaka.

Wakati wa kampeni hii Hizb ut Tahrir itawasilisha mtazamo wa wazi wa Mfumo wa Kiislamu juu ya masuala yanayohusiana na familia pamoja na kuukumbusha Umma wa Kiislamu katika kushikilia Shakhsiya ya Kiislamu. Tunaamini kwa uthabiti kuwa kukosekana kwa utekelezaji wa Uislamu kama mfumo kamili wa maisha kumesababisha kuzorota sio tu muundo wa kijamii bali kisiasa na kiuchumi pia. Ni Uislamu ambao ulipotekelezwa kwa karne 13 na Khilafah ulitatua changamoto zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pia tunaamini kwamba mara tu Khilafah itakaposimamishwa kwa Njia ya Utume matatizo yote yatatatuliwa.

Amali za kampeni zitajumuisha darsa, mazungumzo ya mitaani, semina na wasomi miongoni mwa nyengine.

Tunatoa wito kwa umma kwa jumla na hasa Umma wa Kiislamu kuungana nasi katika kampeni hii tukufu ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu (swt). Tunamuomba (swt) aifanikishe kampeni hii na kuifanikisha kwa Ummah mzima wa Kiislamu.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir**

**Kenya**

# HABARI NA MAONI
# Kuchaguliwa tena kwa Trump: Mporomoko wa Demokrasia uso Kifani

**Habari:**

Mnamo Novemba 6, 2024, ilithibitishwa kuwa Donald Trump, mhalifu aliyepatikana na hatia, alishinda tena uchaguzi wa rais nchini Marekani. Tukio hili sio tu suala la mtu wa kuchukiza, bali ni dalili ya uozo wa kina katika mfumo wa kidemokrasia wa Magharibi. Huku ulimwengu ukitazama, kuchaguliwa tena kwa Trump kunafichua udanganyifu mwingi ambao demokrasia ya Magharibi imeunadi kwa ulimwengu kwa miaka mingi.

**Maoni:**

Uozo wa Kidemokrasia

Trump daima amekuwa akuwa na sifa ya kiburi, ubaguzi na ubinafsi. Kuregea kwake madarakani nchini Marekani kunadhihirisha mgogoro mpana wa uongozi ambao sio tu unatishia Amerika lakini pia unahujumu fahamu nzima ya demokrasia ya Magharibi. Wakati mhalifu aliyepatikana na hatia na mtu mpotovu waziwazi anaweza kuwekwa kuongoza nchi yenye nguvu zaidi ulimwenguni, kwa mara nyingine tena inafichua jinsi demokrasia ilivyo tepetevu, fisadi, na yenye uwezo wa kutumiwa vibaya. Ule unaoitwa utawala wa watu unasimama wazi zaidi kuliko hapo awali kama jukwaa la watu wenye kiburi, maslahi makubwa, na kipote cha wabaguzi ambao hawajali mahitaji ya kweli ya watu. Kipote hicho hudhibiti simulizi na mtiririko wa pesa, huku watu wakipotoshwa kuamini kuwa wana ushawishi wa halisi. Yale yanayoitwa maadili ya kidemokrasia si chochote ila ni udanganyifu unaotumiwa kuendesha, kudhibiti, na kukoloni watu na mataifa. Hili si jambo la Marekani pekee—linaonyesha uozo jumla wa demokrasia na mgogoro mkubwa wa uongozi katika nchi za Magharibi.

Uhuru, haki, na utu kwa muda mrefu zimekuwa kauli mbiu za Magharibi, lakini ukweli umethibitishwa kuwa na kitu cheusi zaidi. Ulimwengu wa Magharibi haujawahi kuwa mdhamini wa haki au utu; kinyume chake, kihistoria umetumia vyombo vyake vya nguvu kukandamiza, kutawala, kukoloni na kuharibu mataifa mengine. Unaendelea kufanya hivyo leo. Si mfumo unaowalinda wanyonge au unaojali manufaa ya binadamu wote. Badala yake, ni mfumo uliobuniwa kulinda kipote cha mabepari waliobahatika na kudumisha hali halisi iliyopo ambayo inahifadhi utawala wa Magharibi juu ya sehemu zengine za ulimwengu.

Mfumo Mpya wa Kisiasa Unahitajika

Kwa Umma wa Kiislamu, tukio hili ni ukumbusho kwamba hatuwezi kuweka matumaini na mustakabali wetu katika mikono ya dola za Magharibi au viongozi wao, kama baadhi, kwa bahati mbaya, walivyoamini. Wakati Waislamu mjini Gaza wanakabiliwa na mauaji ya halaiki, mara kwa mara tunaona jumuiya ya kimataifa ikifumbia macho.

Ikiwa tunataka kuwasaidia Waislamu nchi Palestina, haitakuwa kupitia Ikulu ya White House! Ni wakati sasa wa kugeuka ndani na kuunda upya mifumo yetu wenyewe kwa misingi ya haki, huruma na umoja. Khilafah ya Kiislamu si ndoto—ni wajibu wa Mwenyezi Mungu na hitaji la kivitendo, ikiwa tunataka kuona uadilifu na utu wa mwanadamu vikipewa kipaumbele katika ulimwengu huu. Hatima yetu haiwezi kutegemea matokeo ya uchaguzi jijini Washington au Paris bali lazima ijengwe kwa nguvu na ukinaifu wetu wenyewe.

Huku Magharibi ikiyumba chini ya uzito wa migongano na migogoro yake, sisi, kama Waislamu, tunayo fursa ya pekee ya kufufua zama za dhahabu ambapo Khilafah ilikuwa ni mwenge wa uadilifu, utu na maendeleo kwa ulimwengu mzima. Ukombozi wa Palestina na ulinzi wa wanyonge mjini Gaza na kwengineko unaweza kutokea tu kupitia Umma wa Kiislamu ulioungana chini ya uongozi wa Khilafah. Ndilo suluhisho—sio kwa Waislamu tu bali kwa wanadamu wote, ambao wanazidi kuteseka chini ya utawala na dhulma ya mfumo wa Magharibi.

Umma wa Kiislamu ndani yake wenyewe una masharti yote ya kuchukua vazi la uongozi. Ni wakati sasa wa Waislamu kuinuka, kukataa mfumo wa sasa wa kisiasa, na kuwa nuru inayowaonyesha wanadamu njia ya kuelekea kwenye jamii adilifu, yenye msingi wa sheria za mungu na uadilifu wa kimaadili.

**[وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُم فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا]**

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote." (Surah An-Nur, 24:55)

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya**

**Hizb ut Tahrir na**

**Ibrahim Atrach**

# Udanganyifu wa Chaguo: Kwa nini Upigaji Kura katika Mfumo wa Kisekula Unawabwaga Waislamu




Kila baada ya miaka minne, uchaguzi unapokaribia, shauku kubwa ya kupiga kura hufurika kwenye vyombo vya habari, washawishi wa mitandao ya kijamii na mashirika mbalimbali. Waislamu pia wanahimizwa kushiriki, mara nyingi kupitia mashirika ya Kiislamu ya ndani. Kwa zaidi ya miongo miwili, wamehimizwa kupigia kura vyama maalum au watu binafsi, wakitumaini kupata manufaa au kuzuia madhara. Mnamo 2000, Waislamu walihimizwa kumpigia kura George W. Bush, ambaye alianzisha Vita dhidi ya Ugaidi, na kuharibu ardhi za Waislamu na kusababisha vifo vya Waislamu karibu milioni 1. Mnamo 2008, Waislamu walimuunga mkono Barack Obama, wakitarajia mabadiliko chanya. Badala yake, Obama alipanua programu za uchunguzi na utegaji za FBI zinazolenga Waislamu nchini Marekani na kuunga mkono madikteta kama Al-Sisi nchini Misri, na kuchochea zaidi migogoro katika Mashariki ya Kati. Mnamo 2020, Waislamu walimpigia kura Joe Biden, ambaye ameunga mkono na kufadhili mauaji ya halaiki huko Gaza huku akiendeleza ajenda ya LGBTQ ndani ya nchi. Hata maandamano ya amani dhidi ya mauaji ya halaiki ya wanafunzi wa asili zote yalikandamizwa kwa usaidizi kutoka kwa Chama cha Kidemokrasia, huku Wana republican wakihimiza ukandamizaji zaidi.

Matukio ya Gaza yanafichua uhalisia wa mfumo wa sasa wa dunia. Mauaji ya halaiki huko, yakiungwa mkono na mataifa yenye nguvu, yanaonyesha jinsi mifumo ya "kidemokrasia" inavyoweza kusaidia ukandamizaji. Uhuru wa maoni huadhimishwa pale tu unapounga mkono mfumo uliopo. Mienendo ya kihistoria inafichua kwamba, bila kujali chaguo la watu wengi, maamuzi mara nyingi yanaegemea maslahi ya kipote cha tawala, na ahadi za uchaguzi zinazotishia maslahi hayo hutupwa mbali haraka. Wananchi wamesalia na mfumo unaodhibitiwa unaowanufaisha wenye nguvu huku ukiweka kando mabadiliko ya kweli.

Sauti za Waislamu, hata hivyo, zina umuhimu kwa watoa maamuzi wa kisekula, lakini hasa kuwaoanisha Waislamu katika usekula, na kuwataka kuacha maadili ya Kiislamu kwa ajili ya kuoanishwa. Mbinu hii inalenga kufuta kitambulisho cha kipekee cha jamii ya Kiislamu, na kuwataka Waislamu kushiriki katika mfumo wa kisiasa wa kisekula ambao hatimaye unahujumu kanuni za Kiislamu.

Wengine wanapendekeza kuwapigia kura wagombea huru ili kuvuruga mfumo wa vyama viwili, wakidhani kuwa inaweza kuwapa Waislamu nguvu. Walakini, uhalisia wa nani anayedhibiti mfumo unabaki. Upigaji kura kwa wagombea huru hutoa tu udanganyifu wa ushawishi katika muundo ulioundwa ili kudumisha mamlaka ya vyama viwili vikuu. Kwa mfano, licha ya mifumo ya vyama vingi vya Ulaya, Waislamu huko wanakabiliwa na sheria kali dhidi ya Uislamu. Mienendo ile ile ya utawala inabakia, bila kujali idadi ya vyama, ikithibitisha Hadith ya Mtume (saw):

«لَا يُلْدَغُ الْمُؤْمِنُ مِنْ جُحْرٍ وَاحِدٍ مَرَّتَيْنِ»

"Muumini hang'atwi mara mbili kutoka kwenye shimo moja." (Al-Bukhari na Muslim).

Waislamu mara nyingi huuliza, "Ikiwa hatutapiga kura, je, tunapaswa kutokuwa wachangamfu kisiasa?" Kinyume chake, Uislamu unawaamuru Waislamu kushiriki kikamilifu na kuendeleza uadilifu ndani ya jamii. Mwenyezi Mungu asema,

***Endelea... UK 5***

[ادْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَادِلْهُم بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ]

"Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora." (Quran, Surah An-Nahl, Ayah 125).
Mtume (saw) akasema zaidi
, «مَنْ رَأَى مِنْكُمْ مُنْكَرًا فَلْيُغَيِّرْهُ بِيَدِهِ فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِلِسَانِهِ فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِقَلْبِهِ وَذَلِكَ أَضْعَفُ الْإِيمَانِ»
"Mwenye kuona uovu miongoni mwenu, na aubadilishe kwa mkono wake; ikiwa hawezi, basi kwa ulimi wake; ikiwa hawezi, basi kwa moyo wake, na hiyo ndiyo imani dhaifu zaidi." (Sahih Muslim).
Uanaharakati wa kisiasa wa Kiislamu hauhitaji ushiriki katika upigaji kura wa kisekula bali ni ushiriki wa vitendo kupitia kuamrisha mema na kukataza maovu.

Kushiriki lazima kuegemee kwenye Aqidah na kuwiana na hukmu za Kiislamu. Upigaji kura katika mifumo inayotunga sheria kinyume na mwongozo wa Mwenyezi Mungu ni haramu, kwani inaidhinisha sheria zilizotungwa na mwanadamu juu ya sheria za Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema,

[أَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ حُكْمًا لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ]

"Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?" (Quran, Surah Al-Ma'idah, Ayah 50).
Uchaguzi wa urais na bunge, ambapo wagombea huidhinisha sheria kinyume na Uislamu, wanalegeza msimamo kwa kanuni za Kiislamu, na kuunga mkono mfumo wa utawala usio wa Kiislamu. Mwenyezi Mungu anaonya,

[وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ]

"Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri." (Quran, Surah Al-Ma'idah, Ayah 44).

Njia bora zaidi kuelekea mbele inaakisi njia ya Mtume Muhammad (saw) na Maswahaba zake, ambao hawakulegeza msimamo kwa maadili ya Kiislamu kwa ajili ya mapato ya muda mfupi. Mwenyezi Mungu ameamuru,

[لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ]

"Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho." (Quran, Surah Al-Ahzab, Ayah 21). Mwongozo huu unawataka Waislamu kuunda Kitambulisho cha kisiasa cha Kiislamu kinachowiana na kanuni za Mwenyezi Mungu.

Jamii ya Kiislamu ina majukumu muhimu, ndani na kimataifa. Ndani ya nchi, Waislamu wanapaswa kuunda majukwaa yao ya kisiasa, si kwa madhumuni ya kupiga kura, bali kuimarisha kitambulisho cha Kiislamu, kujenga mafungamano ya jamii, na kushiriki katika dawah. Kwa kushughulikia masuala ya kijamii kama vile ukosefu wa makao, mwanya wa kiuchumi, na maadili ya kifamilia, Waislamu wanaweza kuonyesha masuluhisho ya Uislamu kwa matatizo ya kijamii, wakiyawasilisha kama jibu kwa changamoto za kisasa. Uwepo imara wa Waislamu, katika jamii na kwenye mitandao ya kijamii, unaweza kushajiisha kutafakari juu ya hekima ya mafundisho ya Kiislamu.

Ulimwenguni kote, Umma wa Kiislamu lazima ushirikiane ili kuregesha umoja na mamlaka, kuondoa ufisadi, na kufukuza ushawishi wa kikoloni. Ruwaza hii inayoegemezwa katika mfumo wa Kiislamu, inalenga kuondosha tawala za kidhalimu na kusimamisha utawala wa uadilifu na huruma wa Uislamu kupitia Khilafah.
Mtume (saw) alibashiri maregeo hayo, akasema:
«ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةٌ عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ»
"Kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya utume." (Musnad Ahmad).
Kusimamishwa tena kwa Khilafah kunaahidi kuhuisha uadilifu na amani, kutekeleza maneno ya Mwenyezi Mungu.

[وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ]

"Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote." (Quran, Surah 21:107).

Kwa kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu, Waislamu wamefaradhishwa kufanya kazi kuelekea ruwaza hii, wakiungana chini ya bendera ya Uislamu kuongoza jamii kwa huruma na uadilifu. Mwenyezi Mungu anakumbusha,

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ]

"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele." (Quran, Surah Al-Anfal, Ayah 24).

**H. 22 Rabi' II 1446 M**

**Ijumaa, 25 Oktoba 2024Hizb-ut-Tahrir**

**Amerika**

# Hukmu ya Miamala ya Kifedha na Kibiashara kupitia Mtandao wa Intaneti



**Swali:**
Assalamu alaikum wa Rahmatullah wa Barakatahu,

Je, ni ipi hukmu ya biashara, kwa mfano, kununua dinari, mafuta, dhahabu nk kwa dolari wakati wa bei nafuu, kisha kuiuza kwa wakati wa bei ya juu ili kupata faida, huku ukijua kwamba yote haya yanapatikana kwenye mtandao, na anaweza kuhamisha pesa benki na kuzitoa wakati wowote anapotaka?

Swali la pili: Je, inahitajika wakati wa kubadilishana sarafu kuzipokea ana kwa ana au inatosha kuzipokea mtandaoni bila mkono?

-Nitaongeza katika swali hili: Je, akinunua mafuta ni lazima apate kuyamiliki na kuyapokea, na je ikiwa atauza bila kumiliki?

Akijua kwamba akinunua mafuta, chuma, dhahabu au pesa hawezi kuzipokea isipokuwa atazibadilisha kuwa dolari na kuzipokea kama dolari. Kwa hivyo ukinunua mafuta, huwezi kuyapokea kama mafuta, lakini yanabadilishwa kuwa dolari.

Imeelezwa pia katika kitabu cha Nidhamu ya Kiuchumi kwamba hairuhusiwi kabisa kuiuzia, na hii ni pamoja na kile anachomiliki lakini hajakipokea, ambacho kinahitaji kumilikiwa kwa ajili ya kukamilisha mauzo, ambayo hukisiwa, kupimwa uzito, na kuhesabiwa. Ama kile kisichohitaji kukitia mkono kwa ajili ya kukamilisha umiliki wake, ambacho hakikisiwi, hakipimwi, wala hakihesabiwi, kama vile mnyama, nyumba, ardhi na mengineyo, basi inajuzu kwa muuzaji kuuza kabla ya kukipokea.

Swali ni: Je, nitawezaje kuhukumu ikiwa kitu kinakisiwa, kupimwa, au kuhesabiwa au la? Alitaja mfano wa kitu ambacho hakikisiwi, kama mnyama au nyumba, lakini mnyama kama kondoo katika nchi yetu tunapomnunua, tunampima na anauzwa kulingana na uzito wake, akionekana kupimika. Kadhalika, nyumba inaitwa ghorofa moja au ghorofa mbili, ikiwa itahesabiwa, je, nitavichukuliaje kuwa ni vitu visivyohesabiwa au kupimwa?

**Jibu:**
Wa Assalamu alaikum wa Rahmatullah wa Barakatahu,

Kuhusu suala la biashara, hapo awali tumejibu swali kama lako, na nimetoa kutoka kwake kile kinachohusiana na swali lako:

[Kuhusu jibu la swali la kwanza, ambalo ni biashara ya mtandaoni, ni kama ifuatavyo:

1- Kuhusu mafuta, swali haliko wazi:

Je! unataka kujaza gari lako kwenye kituo cha mafuta na kadi ya elektroniki na kumpa afisa wa kituo cha mafuta ambaye atajaza gari lako na petroli? Ikiwa ndivyo, basi inaruhusiwa kwa sababu ikiwa utoaji wa thamani kutoka kwa akaunti yako utachelewa kwa siku moja au mbili, basi inaruhusiwa kununua bidhaa hii kwa mkopo bila riba, na wewe kupokea bidhaa (petroli kwa ajili ya gari lako) na achukua thamani mara moja au baada ya siku moja au mbili. Ikiwa uhalisia ni kama huu, basi hakuna

***Endelea... UK 7***

kitu kibaya na hilo.
Hata hivyo, ikiwa lengo lililokusudiwa la biashara ni kununua kiasi kidogo cha mafuta na kisha kuyauza kabla ya kuyapokea, basi hii hairuhusiwi kwa sababu kupokea ni sharti la kuuza bidhaa hizi. Imepokewa kutoka kwa Abu Dawud kutoka kwa Zaid bin Thabit ambaye amesema:

«فَإِنَّ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ نَهَى أَنْ تُبَاعَ السِّلَعُ حَيْثُ تُبْتَاعُ حَتَّى يَحُوزَهَا التُّجَّارُ إِلَى رِحَالِهِمْ»

“Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (ﷺ) amekataza kuuzwa bidhaa zinaponunuliwa, mpaka wafanyibiashara wachukue katika maboma yao”. Yaani bidhaa hizi haziuzwi isipokuwa baada ya kumilikiwa na kupokelewa. Kwa hivyo, kumiliki ni sharti la uhalali wa uuzaji wao isipokuwa kama kuna andiko maalum kuhusiana na bidhaa fulani, basi inaruhusiwa na sio zengine, na hii haikutajwa hapa ... hivyo basi haijuzu kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu.

Lakini ikiwa unamaanisha kuwa mshirika katika kisima cha mafuta kwa kulipa pesa kupitia kadi ya elektroniki kwenye mtandao, basi hii hairuhusiwi kwa sababu visima vya mafuta ni mali ya umma na havina umiliki wa kibinafsi.

Lakini ikiwa unamaanisha kitu chengine, basi fafanua.

2- Biashara ya dhahabu na fedha:

Ama dhahabu na fedha, kuuza na kununua kwa kila moja yao au kwa pesa taslimu lazima kufanyike mkono kwa mkono, kama katika hadith iliyopokelewa na Al-Bukhari na Abu Dawud kutoka kwa Omar: “Dhahabu kwa fedha ni riba isipokuwa ikiwa ni mkono kwa mkono,” ikimaanisha mkono kwa mkono. Kwa hiyo, kununua dhahabu kwa fedha au kwa pesa si halali isipokuwa kwa mkono kwa mkono.

Na kwa sababu baada ya kujifunza jinsi ya kufanya biashara mtandaoni, ubadilishanaji haufanyiki mara moja, lakini badala yake inaweza kuchukua masaa au siku, kwa hivyo hairuhusiwi kununua dhahabu na fedha kwa kadi ya elektroniki kupitia mtandao isipokuwa ikiwa kadi itakatwa kutoka kwa akaunti hapo hapo wakati wa kununua dhahabu au fedha, yaani mkono kwa mkono, hivyo usipokee dhahabu au fedha isipokuwa wakati kiwango cha thamani kitatolewa kutoka kwa akaunti yako. Na kwa kuwa hakuna ubadilishanaji wa hapo hapo katika biashara ya mtandaoni, bali baada ya siku moja au mbili, basi haijuzu.

3-Biashara ya hisa na bondi ni haramu kwa sababu hisa zinatokana na makampuni ya hisa ambayo ni batili kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu, na kwa sababu bondi zinahusishwa na riba, na vile vile katika kitabu Msukosuko wa Masoko ya Hisa na vitabu vyengine, tumetaja katika kijitabu, Msukosuko wa Masoko ya Hisa, mukhtasari wa jambo hili kama ifuatavyo:

“Ama hukmu ya Shari´ah inayohusu kufanya biashara katika hisa hizi na katika dhamana, iwe kununua au kuuza, ni haramu. Hii ni kwa sababu hisa hizi ni za muundo wa kampuni ambayo ni haramu kwa mujibu wa Shari´ah. Kwa hakika ni vyeti vya bili ambazo zina kiasi mseto kutoka kwa mtaji halali na faida haramu inayotokana na muamala haramu. Kila bili inawakilisha thamani ya hisa, na hisa hii inawakilisha sehemu ya mali ambayo ni ya kampuni haramu. Mali hizi zimechanganywa na muamala wa haramu ambao Shari´ah imeharamisha. Kwa hivyo, ni pesa haramu, ambayo kununua na kuuza kunakuwa ni haramu, na kuamiliana na pesa hizo pia ni haramu. Hii pia ndio hali kwa dhamana, ambayo fedha imewekezwa kwa riba, na hivyo ndivyo hali ya hisa za benki na mithili yake, kwa kuwa zote zinajumuisha kiasi cha pesa haramu; hivyo kununua na kuuza kwake ni haramu, kwa sababu pesa zilizomo ndani yake ni haramu.” MWISHO WA NUKUU.

4- Uuzaji wa sarafu za karatasi kwenye mtandao, kama vile dolari na euro, ni marufuku kwa sababu hakuna ubadilishanaji wa mkono kwa mkono, ambao ni muhimu katika kubadilishana pesa. Kubadilishana mkono kwa mkono, kama inavyotumika kwa dhahabu na fedha, pia hutumika kwa pesa za karatasi kwa misingi ya sarafu, yaani kuzitumia kama thamani ya bidhaa na mishahara. Tulitaja yafuatayo katika Jibu la Swali la tarehe 11/07/2004:

[Kuamiliana na sarafu za karatasi

Ndiyo, kinachotekelezeka kwa dhahabu na fedha katika suala la riba na hukmu nyengine za fedha kinatekelezeka kwake pia. Hii ni kwa sababu utambuzi wa sababu (pesa taslim, yaani matumizi yake kama bei na mishahara) katika karatasi hizi huzifanya zichukue hukmu za pesa.

Kwa hiyo, kununua vitu vya riba kwa karatasi hizi kunatekelezeka kwa yale yaliyotajwa katika Hadith (mkono kwa mkono), yaani sio deni.

Mada ni kama ifuatavyo:
Mtume (saw) asema:

«الذَّهَبُ بِالذَّهَبِ، وَالْفِضَّةُ بِالْفِضَّةِ، وَالْبُرُّ بِالْبُرِّ، وَالشَّعِيرُ بِالشَّعِيرِ، وَالتَّمْرُ بِالتَّمْرِ، وَالْمِلْحُ بِالْمِلْحِ، مِثْلًا بِمِثْلٍ، سَوَاءً بِسَوَاءٍ، يَداً بِيَدٍ، فَإِذَا اخْتَلَفَتْ هَذِهِ الْأَصْنَافُ فَبِيعُوا كَيْفَ شِئْتُمْ إِذَا كَانَ يَداً بِيَدٍ»

“Dhahabu ilipwe kwa dhahabu, fedha kwa fedha, ngano kwa ngano, shayiri kwa shayiri, tende kwa tende, na chumvi kwa chumvi, mithili kwa mithili sawa kwa sawa, malipo yafanywe mkono kwa mkono. Ikiwa matabaka haya yatatofautiana, uzeni mupendavyo ikiwa malipo yatafanywa mkono kwa mkono.” (Imepokewa na Al-Bukhari na Muslim kutoka kwa Ubada bin Al-Samit, Mwenyezi Mungu awe radhi naye.)

***Endelea... UK 8***

Andiko liko wazi pindi vigawanyo hivi vya riba (riba) zinapotofautiana, kwamba uuzaji ni kama munavyotaka, yaani, sawa kwa sawa sio sharti, lakini ubadilishanaji ni sharti. Neno "vigawanyo" lilitajwa kwa jumla katika vigawanyo vyote vya riba, yaani sita, na hakuna kinachotolewa humo isipokuwa kwa andiko, na pale ambapo hakuna andiko, hukmu ni kwamba ngano inaruhusiwa kwa shayiri au ngano kwa dhahabu, au shayiri kwa fedha, au tende kwa chumvi, au tende kwa dhahabu, au chumvi kwa fedha ... nk. Haijalishi jinsi thamani ya ubadilishanaji na bei ni tofauti kiasi, lakini mkono kwa mkono, yaani sio deni. Na kile kinachotekelezeka kwa dhahabu na fedha kinatekelezeka kwa pesa za karatasi kwa sababu ya lengo kuwa moja (pesa, yaani, matumizi yake kama bei na ujira).] Mwisho.

Kwa kuchunguza jinsi biashara hii ya mtandaoni ya kununua na kuuza dhahabu inavyofanyika, imebainika kuwa ukusanyaji au malipo hucheleweshwa kwa siku moja au mbili ... kuanzia tarehe ya mkataba, na hii ni kinyume na sharti lililokubaliwa la ubadilishanaji, ambalo Mtume (saw) ameliweka katika kauli yake: "Mkono kwa mkono." Imesimuliwa na Al-Bukhari kutoka kwa Al-Bara' bin Azib, ambaye amesema: Tulimuuliza Mtume (saw) kuhusu hilo, naye akasema:

«مَا كَانَ يَدًا بِيَدٍ فَخُذُوهُ وَمَا كَانَ نَسِيئَةً فَذَرُوهُ»

"Chukueni kile ambacho ni mkono kwa mkono na acheni kile ambapo ni kwa mkopo." Muslim amepokea kutoka kwa Malik bin Aws bin al-Hadathan kwamba amesema: Nilikuja na kusema: Ni nani anayebadilishana dirham? Talha ibn Ubaydullah akasema alipokuwa na Umar ibn al-Khattab: Tuonyeshe dhahabu yako, kisha uje kwetu atakapokuja mtumishi wetu na tutakupa pesa zako. Umar bin al-Khattab akasema: Hapana, Wallahi ni lazima ima umpe pesa zake au umrudishie dhahabu yake, kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: «الْوَرِقُ بِالذَّهَبِ رِبًا إِلَّا هَاءَ وَهَاءَ...» "Dhahabu na fedha ni riba, isipokuwa hii kwa hii..."

Kutokana na hayo, hairuhusiwi kufanya biashara ya euro, dolari na aina nyingine za sarafu kwenye Mtandao kwa sababu hakuna ubadilishanaji wa hapo kwa hapo)] Mwisho wa kunukuu.

Kuhusiana na swali lako kuhusu bidhaa zenye kukisiwa, kuhesabiwa na kupimwa, nyuma tulijibu swali kama hilo kama ifuatavyo:

Jibu la Swali la tarehe 12/02/2006, ambalo lilisema: [Kuhesabiwa, kupimwa na kukisiwa ni kulingana na uhalisia wa uuzaji wa bidhaa.

...Angalia sokoni uone hii bidhaa inauzwaje? Je, inauzwa kwa idadi, maana yake inasemwa sokoni kila nafaka kwa bei hii au kila moja kwa bei hiki? Je, inauzwa kwa uzito, kwa hiyo inasemwa kila kilo kwa bei hii? Au inasemwa kila mita kwa bei hii? Au kila saa' (aina ya kipimo kikavu) kwa bei hii?...

Ikiwa ni hivyo, maelezo ya kuhesabiwa, uzito au kipimo yanatekelezeka kwake, iwe ni maelezo ya kimoja au zaidi, kumaanisha kuwa bidhaa hiyo inaweza kusifiwa kuwa ni yenye kupimwa na kuhesabiwa...

Mifano: ngano, shayiri ... kwa uzito na kipimo.

Ndizi, machungwa... kwa uzito na kwa idadi (katika baadhi ya nchi huuzwa kwa idadi)...

...na kuamua maelezo yake wakati wa kuvichukua vitu hivi ni muhimu ili kuondoa ujinga. Mtu anaponiambia kuwa nina kilo 100 za ngano, haitoshi kuamua maelezo. Badala yake, aina ya ngano lazima ielezwe ili uzito uondoe ujinga, na vilevile kwa kipimo na kuhesabiwa.

Lakini je, mnyama anauzwa kwa idadi, ili hata itangazwe kila ngamia mmoja kwa elfu, au anauzwa kupitia mnunuzi kumuona na kumtazama na kusema ngamia huyu hana thamani ya elfu moja kisha amchague ngamia wa pili? Je! kila ngamia ni kama mwenzake kiasi kwamba mauzo ni kwa idadi?

Kisha je, nyumba zinauzwa kwa idadi, uzito, au ujazo? Kwa maana nyengine, je, mtu mwenye nyumba kumi hunadi na kusema, "Nyumba moja ni ya elfu moja," au nyumba yoyote hununuliwa kwa kuiona, na ni tofauti na nyengine...

Kwa hiyo, inasemekana kwamba mnyama na nyumba haziuzwi kwa kipimo, uzito au idadi. Unaweza kusema kwamba baadhi ya watu huuza wanyama wao kwa uzito, lakini sivyo ilivyo kwa kila mnyama. Anaweza kuuza kondoo fulani kwa kutumia uzito, lakini hauzi kila kondoo, wala hauzi kila mnyama, kwa hivyo hauzi ng'ombe kwa uzani ... kwa hivyo haisemwi kwangu, chukua kilo mia za wanyama (bila shaka, kumaanisha wako hai).

Vivyo hivyo, unaweza kusema kwamba baadhi ya watu huuza nyumba kwa mita, lakini hii haitumiki kwa kila nyumba. Badala yake, mita katika nyumba hii ni kumi, na katika nyumba ile ni ishirini, na kadhalika. Kwa hiyo, maelezo sahihi kwake sio kwa kipimo, kwa hivyo haisemwi kwangu, chukua nyumba ya mita mia moja

... Na kadhalika....] Mwisho.

Natumai hili linatosheleza, na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi na ni Mwingi wa Hekima.

**Ndugu Yenu,**
**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
**11 Rabi' al-Akhir 1446 H**
**Sawia na 14/10/2024 M**